**PRIMARY EDUCATION SERVICES NETWORKING ORGANIZATION (PESNO)**

**SIMU: 0713- 526533**

**0767- 526533**

# MTIHANI WA KWANZA WA UTAMILIFU KWA DARASA LA SABA

## SOMO: SAYANSI [05]

**TAREHE 09/03/2021 MUDA: SAA 1:30**

**JINA LA MTAHINIWA:** ______________________________

**JINA LA SHULE:** ______________________________

**WILAYA**: __________________ **MKOA:** __________________


## MAELEKEZO:

1. Jaza nafasi wazi hapo juu na katika karatasi ya majibu
2. Jibu maswali yote kwa kufuata maelekezo katika kila sehemu.
3. chagua jibu sahihi kisha siliba herufi yake katika karatasi ya kujibia (OMR)kwa kutumia kalamu ya risasi kuanzia swali 1 hadi 40
4. Katika swali la 41 hadi 45 jibu maswali kwa kuandika majibu nyuma ya karatasi ya (OMR)
5. Hakikisha kazi yako iko nadhifu na safi
6. Mtihani huu una kurasa nne zilizochapishwa


**SEHEMU A: MACHAGUO**

1. Ipi kati ya zifuatazo ndio sehemu kuu za mmea?
   a. shina, majani, maua b. maua, matawi, majani c. mizizi, majani, shina d. kotiledoni, mizizi, majani e. mmea, maua, kotiledoni
2. Magonjwa mengi katika mazingira yetu huweza kuepukwa kwa:
   a. kutengeneza dawa za kutosha b. kuunguza taka c. usafi d. kuwa na kiboksi cha huduma ya kwanza e. kujenga hospitali nyingi
3. Ili kuzuia upungufu wa damu kwa mama mjamzito anatakiwa kula chakula chenye:
   a. fati b. protini c. maji d. madini e. wanga
4. Nini kazi ya chembe sahani katika mwili?
   a. kusafirisha hewa ya oksijeni b. kusafirisha taka mwili c. kuulinda mwili zidi ya magonjwa d. kusafirisha kemikali katika mwili e. husaidia kugandisha damu na kuponya majeraha
5. Taka mwili zilizochujwa na figo husafirishwa kwenda kwenye kibofu cha mkojo kupitia mirija iitwayo:
   a. urethra b. ureta c. ateri ya renali d. vena ya renali e. bronchioli
6. Ni mnyama yupi kati ya hawa hatagi mayai?
   a. popo b. chura c. samaki d. mamba e. mjusi
7. Ni sehemu gani ya ua uendelea kukua na kuwa tunda?
   a. petali b. stameni c. ovari d. stigima e. kikonyo
8. Ni gesi ipi huongezwa na mimea wakati wa mchana?
   a. naitrojeni b. kabonidayoksaidi c. kabonimonoksaidi d. haidrojeni e. oksijeni
9. Mpangilio upi ni sahihi katika uandishi wa ripoti ya kisayansi?
   a. lengo, hatua,matokeo, mahitaji, hitimisho
   b. hatua, matokeo, lengo, mahitaji, hitimisho
   c. kichwa, lengo, mahitaji, hatua, matokeo, hitimisho
   d. lengo, hitimisho, kichwa, matokeo, hatua, mahitaji
   e. matokeo, lengo, hatua, hitimisho, kichwa, mahitaji
10. Mojawapo kati ya sentensi zifuatazo ni sahihi kuhusu gesi vunde
    a. Imetengenezwa kwa miamba
    b. Inaweza kutengenezwa kwa mavi ya ngombe tu
    c. Inaweza kutengenezwa kwa kinyesi cha binadamu tu
    d. Inaweza kutengenezwa kwa maganda ya mchele
    e. Inaweza kutengenezwa kwa vitu vinavyooza tu
11. Katika makundi yafuatayo ni kundi lipi linalowakilisha mashine tata?
    a. kitasa, baiskeli na saa b. cherehani, baiskeli, mkasi c. mkasi, rula, cherehani d. msumeno, baiskeli, gari e. saa, pikipiki, mkasi
12. Ili tendo la osmosis lifanikiwe, kunahitaji kuwepo na………
    a. kiazi, maji na jiwe b. kiazi, maji na chumvi c. kiazi, kisu na jiwe d. kiazi bila kitu kingine e. kiazi, maji na mchanga
13. Ipi kati ya hizi sio chanzo cha umeme?
    a. upepo b. ngurumo c. maporomoko ya maji d. jua e. mafuta
14. Kwa nini wakati wa kiangazi mimea hupukutisha majani?
    a. kupunguza kupotea kwa maji b. kupunguza kunyonywa kwa maji c. kuongeza rutuba d. kuthibiti fotosinthesis e. kuonesha uwepo wa kiangazi
15. Jinsia ya mtoto inaweza kuwa ya kike kama kromosomu X itaunganika na ________kromosomu.
    a. X b. V c. XY d. Y e. Z
16. Viumbe hai vyote vina tabia zifuatazo isipokuwa tabia moja tu nayo ni………..
    a. Kuzaliana b. kukua c. kusogea toka sehemu moja hadi nyingine d. kuitikia kichocheo e. kutengeneza chakula chake

17. Mchoro huu unawakilisha tendo gani katika mimea?
   a. Haidrotropizim
   b. Fototropizim
   c. Fotosinthesis
   d. Kemotropizim
   e. Jiotropizim




18. Ipi kati ya hizi ni badiliko la kikemia?
   a. maji kuwa mvuke b. asali kuwa pombe c. kusaga mahindi kuwa unga d. kuyeyuka kwa mshumaa e. kuyeyuka kwa sukari
19. Kitu gani kitatokea iwapo utawasha mshumaa na kufunika kwa glasi?
   a. glasi itavunjika b. mshumaa utazima c. mshumaa utakwisha d. mshumaa utaendelea kuwaka e. mshumaa utanata kwenye glasi
20. Nini matokeo ya mwisho katika uyeyushaji wa chakula cha wanga?
   a. asidi za amino b. glukosi c. asidi za fati d. maltosi e. amilosini
21. Wadudu wapi kati ya hawa wafuataο hukua katika metamofosisi kamili?
   a. panzi na kipepeo b. nyuki na mende c. nyoka na panzi d. kipepeo na inzi e. inzi na mende
22. Uwiano kati ya kani ya mzigo na kani ya jitihada huitwa:
   a. manufaa ya kimakanika b. kanuni ya mwendo c. mwendo kasi d. mwendo dhahiri e. mzigo
23. Ni rangi gani hutoa msisitizo wa tabia au kitendo fulani katika alama za usalama katika mazingira?
   a. njano b. kijani c. nyeusi d. bluu e. nyeupe
24. Ni kifaa gani katika runinga au radio hufanya sauti isikike vizuri au picha kuonekana vizuri?
   a. betri b. skrini c. antenna d. spika e. nyaya
25. Joto husafiri katika maada yabisi kwa njia ya
   a. mpitisho b. msafara c. mnururisho d. mitetemeko e. kusharabu
26. Ni kioo gani kinatoa taswira wima inayofanana na kitu halisi na ambayo umbali kati yakioo ni sawa na umbali kati ya kioo na kitu halisi?
   a. kioo cha konkevu b. kioo cha bikonkevu c. kioo cha konveksi d. kioo cha prismu e. kioo cha bapa
27. Magonjwa ya zinaa huambukizwa kwa njia ya ……..
   a. Kujamiiana b. kuchangia vikombe c. kucheza pamoja d. kupeana damu e. kugusana
28. Ni ugonjwa upi hauna chanjo kati ya magonjwa yafuatayo?
   a. polio b. trakoma c. kifua kikuu d. kifaduro e. surua
29. Nini thamani ya X katika mchoro huu?




   a. sm10 b. sm 4 c. sm 0.4 d. sm 0.5 e. sm 6
30. Ni ogani zipi huhusishwa na utoaji taka mwili?
   a. ngozi, figo b. mapafu, moyo c. ini, goita d. bandama, moyo e. tumbo, figo
31. Ni viini lishe gani vinavyopatikana katika vyakula vya kujenga mwili?
   a. fati b. madini c. kabohaidreti d. protini e. vitamini

32. Chunguza kielelezo hiki kwa makini kisha jibu swali lifuatalo.



Kiumbe aliyeoneshwa katika kielelezo hiki huishi kwa kutegemea…..

a. nyama  b. asali  c. nafaka  d. maada zilizooza  e. vyakula vya majini

33. Moja kati ya zifuatazo sio aina ya antenna?

a. waya  b. kidoa  c. spoku  d. safu  e. kipenyo

34. Yapi ni makundi makuu mawili ya viumbe hai?

a. mimea na waduu b. wanyama na samaki  c. mimea na wanyama  d. mimea na binadamu  e. binadamu na wanyama

35. Angalia mchoro ufuatao, mmea gani una mizizi kama iliyooneshwa katika mchoro?



a. mharagwe  b. nyanya  c. mpera  d. Mwembe  e. nyasi

36. Zifuatazo zinaweza kusafirisha kani katika mashine kutoka sehemu moja ya mashine kwenda sehemu nyingine **ISIPOKUWA------**

a. belti  b. mafuta  c. cheni  d. kamba  e. gia

37. Kati ya vifuatavyo ni kipimo kipi kinapima ujazo wa vitu?

a. kilogramu  b. sentimita  c. newtoni  d. lita  e. ampia

38. Ipi kati ya zifuatazo sio dalili za mtu anayeumwa UKIMWI?

a. Homa kali na kukohoa kwa muda mrefu  b. Kukohoa mara kwa mara  c. Kuongezewa damu yenye vvu  d. Kuharisha mara kwa mara na vidonda mdomoni  e. Kupungua uzito na kuchoka

39. Baada ya huduma ya kwanza kwa mtu aliyeumia, mtu huyo anapaswa:

a. apelekwe hospitali  b. apewe mapumziko  d. alazwe chini ya mti  d. apulizwe hewa mdomoni  e. apewe maji ya kunywa ya kutosha

40. Tarakilishi mbili au zaidi zikiunganishwa kwa lengo la mawasiliano huunda……….

a. modemu  b. runinga  c. radio  d. mtandao  e. google chrome

**SEHEMU B: MAJIBU MAFUPI**

41. Tafuta densiti ya kitu chenye tungamo gramu 152 na ujazo wa sentimeta 20

42. Mkondo wa umeme wa ampia 0.6 unapita katika waya wenye ukinzani wa ohm20. Tafuta tofauti ya potenshali kwenye waya.



43. Alama hii katika usalama kwenye mazingira huwakilisha nini?

44. Virusi vinavyosababisha ukimwi vikiingia mwilini hushambulia seli zinazoitwa……………

45. Nini kitatokea kwenye miche ya sumaku hii kama itasogezwa karibu?

